

Ghorofa ya 7, Jengo la Mfuko wa LAPF, Mkabala na Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama
S. L. B. 72175, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255-22 2923513-18; Nukushi: +255-22 2923519 Website: www.ewura.go.tz

**ONGEZEKO LA MUDA WA USAJILI KWA WANANCHI WENYE UWEZO
WA KUUZA BIDHAA NA KUTOA HUDUMA KWENYE KANZIDATA ILI
WASHIRIKI KWENYE SHUGHULI ZA PETROLI KWA MWAKA 2018**

1. Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inasajili wauzaji wa bidhaa na watoa huduma mbalimbali kwenye kanzidata ya Watanzania wenye uwezo katika sekta ndogo ya petroli, mkondo wa kati na wa chini, nchini Tanzania.

2. Usajili wa wananchi wenye uwezo wa kuuza bidhaa na kutoa huduma kwenye kanzidata ya LSSP ni kwa mujibu wa Kanuni ya 38 ya Ushirikishwaji wa Wananchi za mwaka 2017. Dirisha la usajili lilifunguliwa tarehe 29 Januari 2018 kwenye tovuti ya EWURA.

3. EWURA imegundua kuwa Watanzania wengi wenye nia ya kujisajili kwenye kanzidata bado wanahangaika kujaza fomu na kutafuta viambatisho husika. Aidha, EWURA imepokea maombi ya Watanzania kutaka kipindi cha kuwasilisha maombi ya usajili kiongezwe. Baada ya kutafakari kwa mapana maombi hayo na lengo la kuwa na kanzidata, EWURA imekubali kuongeza kipindi hicho kutoka tarehe **28 Februari, 2018 hadi tarehe 31 Machi, 2018**.

4. Mamlaka inaendelea kupokea **maombi** yanayowasilishwa **KIETRONIKI PEKEE** kupitia anwani ya barua pepe. Mwananchi yeyote au kampuni yenye nia ya kuwasilisha maombi ya usajili anakaribishwa kupata taarifa kwenye tovuti ya EWURA: www.ewura.go.tz bonyeza kwenye maandishi: **LOCAL CONTENT DATABASE** kuona maelekezo ya jinsi ya kujaza Fomu N-100. Maombi yote yawasilishwe kupitia anwani ya info@ewura.go.tz kabla ya saa 5:59 usiku wa tarehe 31 **Machi 2018**.

5. Mwenye maswali kuhusu jinsi ya kujisajili huo ayawasilishe EWURA wakati wa saa za kazi (02:00 hadi 11:00 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa) kwa anwani ifuatayo-

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
7th Floor, Jengo la Mfuko wa LAPF,
Mkabala na Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama,
S. L. B. 72175, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2923513-18; Nukushi: +255-22 2923519
Barua pepe: info@ewura.go.tz
Tovuti: www.ewura.go.tz